**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI INYONGA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI INYONGA**
**S.L.P 46, MLELE - KATAVI**
***Na. ya simu 0757682461,***
***Mkuu wa Shule: 0787137188***
**TAREHE:……………………**

**Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi:- …………………………………………………………….**
**S.L.P ……. Mji/Wilaya………………………………. Mkoa……………………………….**
**Namba ya simu………………………………..**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI INYONGA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE MKOA WA KATAVI MWAKA………………………**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ……. na atasoma tahasusi aliyochaguliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI.

**2.** Shule ya Sekondari Inyonga ipo kaskazini mwa Mji wa Inyonga, Halmashauri ya wilaya ya Mlele, Mkoa wa Katavi. Kwa usafiri wa basi shule inafikika kutoka mjini Mpanda kuja Inyonga-Mlele na unapatikana katika kituo cha mabasi Mpanda. Kutoka mjini Tabora kuja Inyonga unapatikana mjini Tabora. Kutoka kituo cha mabasi Inyonga kuja shuleni kuna umbali wa kilometa 2 na usafiri ni wa pikipiki (bodaboda) na bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe …………. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shule tarehe ………………

**3. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**3.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule kwa **wasichana** ni Sketi za darasani mbili (2).Sketi rangi ya khaki draft moja (1) yenye linda ndogo na Sketi rangi ya udongo moja (1) mshono wa solo (kukata) ndefu inayofika kwenye kisigino.

   Sare kwa **wavulana** ni Suruali mbili (2) za darasani, Suruali rangi ya khaki (1) na suruali nyeusi moja (1) kwa Wavulana, yenye marinda mawili na pindo chini.

ii. Mashati meupe mawili (2) yenye mikono mirefu isiyo na urembo wowote pamoja na T-shirt moja (1) moja rangi ya bluu yenye nembo. (kwa anayehitaji **inapatikana shuleni).**

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe inayofunika kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama;

iv. Sare ya Michezo ni T-shirti ya njano isiyo na kola yenye nembo, kwa wasichana na kwa wavulana (kwa anayehitaji **inapatikana shuleni**).

v. Kiatu cha raba na bukta rangi ya kijani kwa wavulana na wasichana ni traki suti ya bluu kwa ajili ya michezo.

vi. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

vii. Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.

viii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.

ix. Sweta moja rangi ya kijani choroko mpauko (inapatikana shuleni)

x. Nguo za kushindia (shamba dress).

   Sketi rangi nyekundu ya miraba(draft) ndogondogo mshono wa solo ndefu inayofika kwenye kisigino kwa wasichana. **(kwa anayehitaji inapatikana shuleni).**

   Suruali rangi ya udongo kwa wavulana na T-shirt moja (1) rangi ya kijivu yenye nembo kwa wavulana na wasichana**. (kwa anayehitaji inapatikana shuleni).**

xi. Kila mwanafunzi aje na lita mbili za dawa ya kusafishia vyoo.

**3.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -**

i. Madaftari ya kutosha kulingana na uhitaji wa tahasusi aliyopangiwa.

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka.

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology pamoja na Lab Coat (**ni muhimu zingatia**).

v. Scientific Calculator kwa tahasusi za CBG na EGM;(**zinapatikana shuleni).**

vi. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni lenye vipimo vya Futi "2 $\frac{1}{2}$ "kwa "6".

Mashuka Jozi 2 rangi ya kijani, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi nyeupe.

vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Mopa 1, jembe 1, na kwanja 1 kwa wanafunzi wa CBG na EGM, reki 1, mifagio 2 (ya ndani soft 1 na hard boom 1) pamoja na chelewa 1 kwa wanafunzi wa HGK na HKL.

**Kumbuka;**
**Kuondoa utata na usumbufu wa rangi na mashono,hizi sare zote za shule zinapatikana maeneo ya shule.**

**3.3 Michango mbalimbali.**

**i. Mchanganuo wa michango**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000.00 |
| 2. | Tahadhari | 5,000.00 |
| 3. | Nembo | 5,000.00 |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000.00 |
| | **Jumla** | **80,000.00** |

Michango yote iliyotajwa hapo juu ilipwe kwenye akaunti ya shule
Namba **61901200067** katika benki ya **NMB**, Jina la akaunti **INYONGA SECONDARY SCHOOL CAPITATION ACCOUNT** (Tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip na aje nayo shuleni).

**MATIBABU:** Kwa mwanafunzi ambaye hana kadi ya Bima ya Afya, anatakiwa kuja na fedha kiasi cha **Sh. 50,400.00** kwa ajili ya kuandaliwa na kupatiwa kadi ya Bima ya Afya kwa wanafunzi. Fedha hii pia iingizwe kwenye akaunti ya shule hapo juu ili kurahisisha upatikanaji wa kadi hiyo.

## SHERIA ZA SHULE:

i. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
ii. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi**

**kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**


i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**



**Mkuu wa Shule**
**Jina la Mkuu wa Shule: PATRICK U. KAPITA**




**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**ANGALIZO: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0757682461**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0756231611**
- **Mwandamizi Taaluma: 0622946571**
- **Mwandamizi Malezi: 0755313043**
- **Matron/Patron: 0765709748 au 0755313043**

Fomu Na ‘1`

INYONGA SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 46,
MPANDA-KATAVI

**FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical officer in respect to all form of entrants Student’s full name …………………………………………………………………

Age ……………………Sex………………………Blood count (red and whites) …………………………………………………………………… Stool examination ……………………………………………………………………………Urine analysis Syphilis and other venereal diseases test ………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

T.B test ……………………………………………………………………………………………

Eye Test ……………………………………………………………………………………….

Ears …………………………………………………………………………………………….. ……………………………………………………………………………………………………………Abdomen

……………………………………………………………………………………………

Urine for plant test……………………………………………………………………………………… ADDITIONAL INFORMATION Defects, impotents (e.g. arms, legs etc) infections, chronic or family diseases etc

…………………………………………………………………………………………………………………… ….

………………………………………………………………………………………………………………………………I certify that the named above is fit to pursue further studies in agricultural/domestic education Station …………………………………………………………..

Signature ………………………………………….

Date. ………………………………………………

Designation ……………………………………….

Fomu Na ‘2’

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE**
**SHULE YA SEKONDARI YA INYONGA**

HISTORIA YA WAZAZI NA MTOTO ALIYECHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE HII

A. WAZAZI/WALEZI

1. Jina la Baba ………………………………….. Hai ☐ Si hai ☐
2. Jina la Mama …………………………………Hai ☐ Si hai ☐
3. Kama Baba si hai,Jina la mlezi ni ……………………………………………………………
4. Kazi/Shughuli ya Mzazi/Mlezi …………………………………………………………………..
5. Anwani ya Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………………………
6. Uraia wa wazazi -Baba Mtanzania ☐ Si Mtanzania ☐
   -Mama Mtanzania ☐ Si Mtanzania ☐
7. Wakati wa likizo Mwanafunzi unataka aende wapi?
   ………………………………………………………………………………..
8. Jina la mtu aendako …………………………………………………….
9. Uhusiano na mwanafunzi. ……………………………………….

SAHIHI YA BABA/MLEZI ………………………. TAREHE…………..
SAHIHI YA MWANAFUNZI…………………….. TAREHE…………

Fomu Na‘3’

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE**
**SHULE YA SEKONDARI INYONGA**

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Mimi ………………………………………………………………………… nimesoma kwa makini maagizo yote na ninatambua kuwa kuchaguliwa kwangu kuingia shule ya Sekondari Inyonga ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa wameshindwa ila kwa sababu ni chache. Hivyo nakubali kujiunga na shule ya Sekondari Inyonga. Nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za Shule. Nitajitahidi kufanya kazi/kusoma kwa juhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikiana na wenzangu kweli daima. Nitalinda hadhi/heshima ya Shule na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shule.

Tarehe …………………………..
Sahihi ya mwanafunzi ……………………………………………
Mimi…………………………………………………………….
Mzazi/ Mlezi wa …………………………………………..

Nimeshuhudia mtoto wangu ……………………………………….. akikubali kwa hiari kujiunga na shule hiyo ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi kikamilifu katika kumlea kijana wangu naamini tutakuwa tunawasiliana.
Tarehe ………………………………………………………
Sahihi ya Mzazi/Mlezi …………………………………………………..

Fomu Na "4"

**PICHA ZA WAZAZI NA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI**

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………………TAHASUSI: [ ]

| PICHA 1<br>Bandika picha hapa | PICHA 2<br>Bandika picha hapa |
|---|---|
| JINA:………………………… | JINA:………………………… |
| UHUSIANO………………… | UHUSIANO……………….. |
| NAMBA YA SIMU…………….. | NAMBA YA SIMU……………. |

| PICHA 3<br>Bandika picha hapa | PICHA 4<br>Bandika picha hapa |
|---|---|
| JINA:………………………… | JINA:………………………… |
| UHUSIANO……………….. | UHUSIANO……………….. |
| NAMBA YA SIMU……….. | NAMBA YA SIMU…………….. |